

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda baiskeli Dar es salaam
28 April 2007**

Waliohudhuria

Abdallah Khatib

Elaine Baker

Juma Ali Salehe Jongo

Jumanne Idd

Kibwana Mohammad Msiga

Paulo Atibu

Mafuta na mikokoteni

Eleine aliripoti kuwa aliandika barua kwa halmashauri ya manisipaa ya ilala na meya wa ilala kuomba mkutano zaidi kwa mapendekezo yetu ya kutatua tatizo la msongamano barabarani, kama ilivyokubalika kwenye mkutano uliopita wa UWABA. Aliwasilisha barua hiyo tarehe 19 Aprili na meya alikuwa ofisini aliongea nae kuhusu uamuzi juu ya mafuta na mikokoteni. Meya alisema kuwa uamuzi ungetolewa baadae na halmashauri.

Paulo alikuwa kwenye mkutano ulioitishwa na meya mapema siku hiyo (28 April). Kulikuwa na kutokuelewana kwa simu kabla ya siku hiyo. Paulo alipowapigia simu watu akiwaambia kuhusu mkutano na meya wao walidhani ni mkutano wa UWABA, hivyo hawakujua kuhusu mkutano na meya. Pia ofisi ya meya haikuwapigia simu Elaine au mejah, kuwajulisha kuhusu mkutano ingawa namba zao za simu walikuwa nazo. Mkutano ulitangazwa kwa kipaza sauti kariakoo.

Paulo aliripoti kuwa meya alitangaza kuwa wamejadili mawazo yaliyotelewa na UWABA na kuamua kuwa maguta na mikokoteni yaendeleo kutumika. Meya alitangaza kuwa kila kikundi cha wadau wa sekta ya usafirishaji waunde kikundi na wachague viongozi. Viongozi hao ndio watakaalikwa kujadili tatizo la msongamano barabarani na masuala mengine ya usafirishaji. Mkutano utafanywa jumanne tarehe 15 Mei

Iliamuliwa kuitisha uchaguzi kwa kamati ya UWABA jumamosi itakayofuata, kwani wako baadhi ya wajumbe wa UWABA ambao sio wanakamati lakini wako hai ile hali wapo wajumbe wa kamati lakini hawako hai kwenye utekelezaji

Iliamuliwa kwamba wanachama wa UWABA watoe taarifa walizozipata kwa vipaza sauti, radion au magazetini kuhusiana na kazi za UWABA, kwenye kamati ili azisambaze kwa wajumbe wengine na pia meya wa ilala aombwe kuwasiliana nasi na kutangaza mkutano kwa vipaza sauti.

Mkutano na Profesa Rwebangira.

Elaine aliripoti kuwa amepewa anauani ya pProfesa Rwebangira na Robert ujerumani. Profesa Rwebangira anafundisha chuo kikuu cha Dar es Salaam na ni mhandisi anayependelea vyombo vya usafiri visivyo vya moto. Elaine alikutana nae siku moja chuoni hapo wakati wa chakula cha mchana. Alitoa nakala ya kitabu cha “productive and liveable cities – Guidelines for pedestrian and bicycle traffic in African Cities”. Ilipendekezwa kuwa aalikwe ili kutoa ushauri kwenye mkutano wa UWABA.

Msafara wa Baiskeli

Wawakilishi wa CHABADA hawakuweza kufika kwenye mkutano wa UWABA, wawili kati yao (CJax na Kandile) walipigia Elaine simu nyumbani kwake, walisoma mchanganuo kuhusu msafara na kuongeza maoni yao ikiwemo pendekezo la kuwa na kamati rasmi ya maandalizi yenye wajumbe watatu. Elaine alituma barua pepe kwa Bradley na alikutana nae Cape Town alipokwenda kikazi. Bradley alisema kwamba bwana Nyoni ni mwakilishi wa ITDP Tanzania na lilikuwa pendekezo lake la kutumia bajeti ya ITDP kwa Tanzania. Pia alipendekeza kutohusisha msafara wa baiskeli na msongamano wa baiskeli ambao ni hatarishi. Alipendekeza kuwa tutoe ufafanuzi wa wajibu wa kila kikundi. Alisema amemtumia Bwana Nyoni mapendekezo ila Elaine alipomuuliza Bwana Nyoni alisema hajaipata. Eline atamtumia tena wiki ijayo.

Ukarabati wa Barabara za Sam Nujoma, Nelson Mandela na Kilwa.

Mkutano ulifikiria kuhusu habari tunazohitaji kuhusu mipango ya barabara hizi na kujiuliza yafuatayo

- Je baiskeli, baiskeli za walemavu, maguta, mikokoteni waenda kwa miguu na magari yanategemewa kupita wapi?
- Je barabara ni pana kiasi gani?
- Je ni namna gani vituo vya mabasi vimepangiliwa na namna gani baiskeli zitapita katikati ya watu wanaosubiri mabasi vituoni.
- Je njia za kuingia pembeni mwa barabara zimepangwa vipi?
- Makutano ya barabara yamepangwa vipi?
- Vizuizi gani vimewekwa kulinda waenda kwa miguu au baiskeli kwa magari na vizuizi gani vimewekwa kuzuia magari kutumia nafasi yasiyoruhusiwa au kukwepa foleni. Ni jinsi gani vinaweza kuvunjwa?
- Je kuna miti?
- Je kuna taa mitaani?

Mengineyo

Wanachama waliomba kupewa nakala za nyaraka mauhimu za UWABA: kama vile cheti cha usajili, na orodha ya wanachama. Baadhi ya nyaraka zinapatikana kwenye tovuti yetu lakini wanachama wengi hawawezi kutumia kompyuta. Elaine alikubali kuchapisha nakala za nyaraka hizo ili zigawanywe. Jumanne pia aliomba fomu tupu ya uanachama ili kuongeza wanachama wengine. Ilikubalika kuwa apewe form lakini wanachama walengwa wawe wapanda baikel na waeleweshwe kuhusu kazi za UWABA na wasisitizwe kuwa hai zaidi.

Juma aliomba taarifa ya mwaka ya UWABA ili aipeleke kwenye ofisi ya usajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali

Mkutano ujao

Ilikubalika kuwa tukutane tena baada ya wiki moja, jumamosi tarehe 5 Mei saa 4 asubuhi. Ajenda kuu itakuwa uchaguzi wa kamati.